

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمُونًا بِكُنُّوْنَ وَعَكِيلُوا الْأَصْبَاحَ كَذَّابِيْنَ لَيَسْتَغْفِفُهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَغْفَفَ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيَمْكُنَنَّ لَهُمْ دِينُهُمُ الَّذِي أَرْضَنَهُمْ وَلَيَجِدُنَّ لَهُمْ مِنْ بَعْدِ حَوْفِيهِمْ أَنَّا  
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Hizb ut Tahrir / Wilayah Bangladesh Imefanikiwa Kuandaa Kongamano la Mtandaoni kwa kichwa: "Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah"

Hizb ut Tahrir / Wilayah Bangladesh, leo Ijumaa, 28 Februari 2020, Imefanikiwa Kuandaa Kongamano la Mtandaoni kwa kichwa: "Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah". Lengo la kongamano hilo ni kuwasilisha kwa Ummah wa Kiislamu, na haswa watu wa nchi hii, kuwa Hizb ut Tahrir imeandaa Kielelezo cha Katiba ya Dola ya Khilafah inayojumuisha vipengee 191 kwa msingi wa Qur'an na Sunnah, ambavyo chama hicho kimejiandaa kikamiliifu kusimamia mambo ya Khilafah ya Uongofu ya pili. Ilijadiliwa katika kongamano hilo jinsi gani Dola ya Khilafah tukufu kwa kutekeleza vipengee vyake vinavyohusiana na katiba hii vitasuluhisha majanga msingi ya hivi sasa ya nchi hii, kama vile: kupata haki msingi za watu (chakula-nguo-malazi, usalama-afya-elimu), kuhakikisha kiwango cha juu cha maisha ya watu na kukuza miundombinu ya nchi.

Serikali ya sasa ya kisekula, katika utawala wake wa miomgo mingi, imeshindwa kutimiza haki msingi za watu, achilia mbali kuhakikisha kiwango cha juu cha maisha. Watu wanaendelea na harakati zao katika barabara dhidi ya serikali kudai haki zao za kimsingi, na serikali inawakandamiza watu kikatili, na kuamua kutumia zana za ubunifu katika ukatili wake. Kwa jina la maendeleo, serikali inafanya miradi mikubwa, yote inajulikana kwa deni kubwa na ujisadi mkubwa, na ambayo hainufaishi watu, lakini badala yake ni mzigo wa madeni makubwa na kodi ya kufadhilli miradi hiyo inaangukia watu. Juu ya watu inatozwa VAT inayoongezeka daima na kodi, na kuongezeka kwa bei ya gesi, maji na umeme. Haya ndiyo matokeo ya nidhamu ya kisekula ya kirasilimali ilioipo, ambapo watawala wana nguvu ya kutunga sheria juu ya maslahi yao wenyewe, na vile vile matamanio yao na tamaa zao. Ambapo, Mwényezi Mungu (swt) asema,

[إِنَّ الْحُكْمَ إِلَّا لِلَّهِ] "Hapana hukumu ila ya Mwényezi Mungu tu" [Yusuf: 40]. Kwa kweli, kwa upande mmoja watawala wa hivi sasa wanatumia nguvu ya madaraka haya kupata maslahi yao, maslahi ya warasilimali wachache na maslahi ya mabwana zao - makafiri wakoloni, na kwa upande mwiningine wanatekeleza dhulma (ukandamizaji) kwa watu wengi. Mwényezi Mungu (swt) asema,

[وَمَنْ لَمْ يَخْفُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ]

"Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwényezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu" [al-Maidah: 45]. Njia pekee ya kutoka katika hili ni kusimamisha tena Khilafah ya Uongofu kwa kuiondoa nidhamu ya kisekula ya kirasilimali na serikali inayotawala hivi sasa. Katika muktagha huu, Hizb ut Tahrir / Wilayah Bangladesh iliandaa kongamano hili la mtandaoni.

Katika kongamano hili, wazungumzaji wameangazia: (1) *Jinsi gani Katiba ya Dola ya Khilafah itakavyo hakikisha haki msingi za watu*, (2) *Jinsi gani Katiba ya Dola ya Khilafah itakavyo hakikisha kiwango cha juu cha maishá ya watu na kujenga miundombinu ilioendelea katika nchi*, na (3) *Khilafah iko karibu na vipi hivi karibuni Khilafah itaunganisha Ummah wa Waislamu*.

Kwa kushiriki katika kongamano hilo, wanaharakati wa Hizb ut Tahrir wamefanya maingiliano makubwa na watu ambao wameunda muitikio mkubwa. Watu wameshiriki katika kongamano la mtandaoni kwa shauku.

Tunawashukuru wote, Mwényezi Mungu awajaze kila la kheri, ambao wamefanya kazi bila kuchoka kufanikisha kongamano hili. Tunamalizia kwa dua kwa Mwényezi Mungu (swt) kuwa harakati ya kusimamisha tena Khilafah ya Uongofu ifikie sehemu inayolenga chini ya uongozi wa Amiri wa Hizb ut Tahrir, Sheikh Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah, kwamba Yeye (swt) aturuhusu sisi kusimamisha tena Khilafah ya Uongofu hivi karibuni kwa msaada na ushiriki mchangamfu wa Ummah wa Waislamu.

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir / Wilayah Bangladesh: [www.ht-bangladesh.info](http://www.ht-bangladesh.info)

[www.hizb-ut-tahrir.org](http://www.hizb-ut-tahrir.org)

Pepe: [contact@ht-bangladesh.info](mailto:contact@ht-bangladesh.info)

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:  
[www.hizb-ut-tahrir.info](http://www.hizb-ut-tahrir.info)

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Bangladesh

Simu\Fax.: 009611307594 Rununu: 0096171724043

Pepe: [media@hizb-ut-tahrir.info](mailto:media@hizb-ut-tahrir.info)

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.org](http://www.hizb-ut-tahrir.org)

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.info](http://www.hizb-ut-tahrir.info)